

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS MAGUFULI KUMPOKEA RAIS MNANGAGWA WA ZIMBABWE KESHO.**

Nchi yetu imepata heshima ya kupokea ugeni wa Mhe. Emerson Mnangagwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Zimbabwe ambaye anatarajiwa kufika hapa nchini siku ya Alhamis tarehe 28/06/2018 kwa ajili ya ziara ya kikazi ya siku mbili kuanzia tarehe 28/06/2018 hadi 29/06/2018.

Mhe. Mnangagwa atapokelewa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere International Airport Terminal I na mwenyeji wake hapa nchini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli muda wa saa 5.00 asubuhi.

Ikumbukwe kuwa hii itakuwa ni ziara ya kwanza kwa Rais Mnangagwa kufika Tanzania kama Rais tokea aingie madarakani mwishoni mwa mwezi Novemba, 2017.

Ujio huu wa Rais Mnangagwa hapa nchini una lengo kuu la kuendelea kudumisha ushirikiano wa muda mrefu uliopo baina ya nchi yetu na nchi ya Zimbabwe tangia wakati wa kupigania Uhuru wa Taifa hili la Kusini mwa Afrika.

Mgeni wetu anatarajiwa kuondoka hapa nchini tarehe 29/06/2018 saa 8.00 mchana na atasindikizwa na mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli.

Kwa kutambua ugeni huu sisi kama wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania tunawakaribisha wageni wetu na wajisikie kuwa wako nyumbani muda wote watakapokuwa hapa jijini.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

27/06/2018